




Ngoma imekuwa ala  
muhimu ya muziki  
katika jamii  
mbalimbali.

Tunazipenda ngoma!  
Tuna ngoma zenyе  
vimoto fauti: kubwa,  
wastani na ndogo.



Tunazicheza ngoma  
kwa kutumia kijiti, au  
kwa kutumia vidole  
vyetu.

Tunazicheza kwa  
sababu tofauti.  
Tunazicheza kwa  
nyimbo na densi,  
wakati wa sherehe na  
wakati wa majonzi.




Ngoma huongeza  
ladha kwenye nyimbo  
na kuwafanya watu  
watake kucheza.  
Ngoma hufanya  
sherehe kuwa  
maridadi.

Tunazicheza wakati wa  
harusi  
na unapompatia  
mtoto jina. Tunacheza  
kusherehekeea mavuno  
au kuzaliwa kwa  
mapacha.




Ngoma hulia  
kutangaza majonzi na  
kuwaita watu  
kunapotokea kifo.



Ngoma hulia kuwaita  
watu kusafisha kisima,  
barabara, au  
kumjengea mtu  
mkongwe nyumba.

Ngoma huwaita watu  
ng'ombe wetu  
wanapokuwa  
wameibwa.



Ngoma hulia kuwaita  
watu wakutane kwa  
chifu wetu.



Ngoma huwaita watu kwenda kanisani kwa maombi siku ya Jumapili, na kwenye siku zingine za maombi.

Pia, ngoma huchezwa kutia ladha wimbo unapoimbwa kanisani.



Ngoma kubwa  
husikika, "An a bul  
mba, an a bul mba, an  
a bul mba-mbamba-  
mba bul." Nayo ndogo  
hutoa sauti ya juu,  
"Tindiri, tindiri tindiri  
ti."

Pamoja zote huitikia,  
"Tindiri mba, tindiri  
mba, tindiri mba-mba-  
mbamba, tindiri ti!"